أصول العقيدة - سواحيلي

# AQEEDAH YA MISINGI




جمعية الدعوة والإرشاد وتوعية الجاليات بالزلفي

297

هاتف: ٤٢٣٤٤٦٦ ٠١٦ ـ فاكس: ٤٢٣٤٤٧٧ ٠١٦

# Misingi ya Aqeedah

## أصول العقيدة - سواحيلي

جمعية الدعوة والإرشاد وتوعية الجاليات في الزلفي
هاتف: 966 164234466 ـ فاكس: 966 164234477

# أصول العقيدة - سواحيلي

## أعده وترجمه للغة السواحيلية

## جمعية الدعوة والإرشاد وتوعية الجاليات بالزلفي

## الطبعة الأولى: ١٤٤٤/٠٦ هـ

ⓗ جمعية الدعوة والإرشاد وتوعية الجاليات بالزلفي ، ١٤٤٤هـ

*فهرسة مكتبة الملك فهد الوطنية أثناء النشر*

جمعية الدعوة والإرشاد وتوعية الجاليات بالزلفي
أصول العقيدة / لغة السواحلية. / جمعية الدعوة والإرشاد وتوعية الجاليات بالزلفي .- الزلفي ، ١٤٤٤هـ
٥٨ ص ؛ ..سم

ردمك: ٠-٠٤-٨٣٩٩-٦٠٣-٩٧٨

١- العقيدة الإسلامية أ.العنوان

ديوي ٢٤٠ ١٤٤٤/٥٨١٥

رقم الإيداع: ١٤٤٤/٥٨١٥
ردمك: ٠-٠٤-٨٣٩٩-٦٠٣-٩٧٨

# Misingi ya Aqeedah.

## أصول العقيدة

## *Tauheed* na Aina Zake

### Maana ya *Tauheed*.

*Tauheed* ni kumpwekesha Allah kwa yale ambayo ni khasa Kwake Yeye, ambayo ni wajibu katika aina zote za ibada. Na hiyo *Tauheed* ni katika jambo kubwa Alililoliamrisha Allah, Allah Anasema katika Qur'an:

قال الله تعالى:﴿قُلْ هُوَ اللَّهُ أَحَدٌ﴾ [الإخلاص:١]

*"Sema Yeye Allah ni Mmoja tu."* (Ikhlas: 1).

وقال سبحانه:﴿وَمَا خَلَقْتُ الْجِنَّ وَالْإِنسَ إِلَّا لِيَعْبُدُونِ﴾ [الذاريات: ٥٦]

Allah Anasema: *"Sikuwaumba majini na binadamu isipokuwa ni kwa lengo la kuniabudu."* (adhDhariyat: 56).

وقال سبحانه:﴿وَاعْبُدُوا اللَّهَ وَلَا تُشْرِكُوا بِهِ شَيْئًا﴾ [النساء:٣٦]

Allah Akasema tena: *"Muabuduni Allah wala msimshirikishe na chochote." (al-Nnisai: 36).*

*Tauheed* imegawanyika vigawanyo vitatu (3);

1. *Tauheed Rubuubiyah* (Ulezi wa Allah)
2. *Tauheed Uluhiyyah* (Uungu wa Allah)
3. *Tauheed Asmai wa Swifat* (Majina ya Allah na Sifa Zake)

## 1: *Tauheed Ar-Rububiyyah*.

Maana yake ni kumpwekesha Allah katika Kuumba na Kuiendesha hii dunia. Na kwamba Yeye Allah Ndiye Mwenye Kutoa Riziki, Mwenye Kuhuisha na Kufisha na Ndiye Mwenye Kumiliki mbingu saba na ardhi saba.

قال تعالى:﴿هَلْ مِنْ خَالِقٍ غَيْرُ اللهِ يَرْزُقُكُمْ مِنَ السَّمَاءِ وَالْأَرْضِ لا إِلَهَ إِلَّا هُوَ فَأَنَّى تُؤْفَكُونَ﴾ [فاطر:٣]

Allah Anasema: *"Hakuna muumba wenu zaidi ya Allah Anayewaruzuku nyinyi kwa mvua kutoka mbinguni, hapana mola isipokuwa Yeye Peke Yake,*

*basi vipi nyinyi mtaepushwa na kumpwekesha?"* (Fatir: 3).

وقال: ﴿تَبَارَكَ الَّذِي بِيَدِهِ الْمُلْكُ وَهُوَ عَلَى كُلِّ شَيْءٍ قَدِير﴾ [الملك:١]

Allah Anasema: *"Ametakasika Yule Ambaye Mikononi Mwake Upo Ufalme wa duniani na Akhera, na Yeye kwa kila jambo ni Muweza."* (Al-Mulk:1).

Na Ufalme Wake Allah ni Ufalme Uliokusanya kila kitu vilivyomo hapa duniani na Kuviswarifu Atakavyo. Ama Kumpwekesha Allah katika Kuendesha mambo yote Duniani ni Kumpwekesha katika Kuumba Kwake.

قال سبحانه: ﴿أَلا لَهُ الخَلْقُ وَالْأَمْرُ تَبَارَكَ اللهُ رَبُّ الْعَالَمِينَ﴾ [الأعراف:٥٤]

Allah Anasema,*"Uumbaji wote ni Wake na ni Yake Yeye Amri, Ametukuka Allah, Bwana wa viumbe wote."* (al-A'raf:56).

Kuendesha mambo kuliko kamilika na kunako kusanya mambo ya viumbe wote.

Na hakuna waliokataa kuamini *Tauheed* hii isipokuwa kundi miongoni mwa wanaadamu, waliikataa hii

*Tauheed* wazi wazi, lakini nafsi zao zilikubali na kuikiri.

قال تعالى: ﴿ وَجَحَدُوا بِهَا وَاسْتَيْقَنَتْهَا أَنْفُسُهُمْ ظُلْمًا وَعُلُوًّا ﴾ [النمل:١٤]

Allah Anasema: *"Na walikanusha Firaun na watu wake, na hali ya kuwa wana yakini ndani ya nyoyo zao, kwa kuifanyia uadui haki na kuwa na kiburi cha kutoikubali." (an-Naml: 14).*

Kupwekesha Peke Yake hakumfai mtu, kama vile ambavyo hawakunufaika washirikina kwa kukiri kwao hii *Tauheed Rububiyyah*.

قال الله عنهم: ﴿وَلَئِنْ سَأَلْتَهُمْ مَنْ خَلَقَ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضَ وَسَخَّرَ الشَّمْسَ وَالْقَمَرَ لَيَقُولُنَّ اللهُ فَأَنَّى يُؤْفَكُونَ﴾ [العنكبوت:٦١]

Allah Anasema: *"Ukiwauliza ewe Mtume hao washirikina, ni nani aliyeumba mbingu na ardhi kwa mpango huu mzuri na akalidhalilisha jua na mwezi, watasema ni alieviumba hivyo ni Allah Peke Yake, basi vipi wao watapotoshwa waache kumuamini Allah." (al-Ankabut:61).*

**2: *Tauheed Al-Uluhiyyah*.**

Maana yake ni Kumpwekesha Allah katika aina zote za Ibada, kwamba asifanye mwanadamu matendo ya kuabudu pamoja na Allah kwa kumshirikisha katika matendo hayo na kiumbe yeyote na pia kujikurubisha kwake huyo kiumbe.

*Tauheed* hii ndio *Tauheed* muhimu sana kuifahamu, ndio *Tauheed* ambayo Allah Amefaradhisha kwa viumbe wote iwe inatekelezwa kwa ajili Yake Allah tu.

قال تعالى: ﴿ وَمَا خَلَقْتُ الْجِنَّ وَالْإِنسَ إِلَّا لِيَعْبُدُونِ ﴾ [الذاريات: ٥٦]

Allah Anasema: *"Sikuwaumba majini na binadamu isipokuwa ni kwa lengo la kuniabudu."* *(adh-Dhariyat: 56).*

*Tauheed* hii ndio ambayo Allah Aliwatuma Mitume Wake kwayo na Akawateremshia na vitabu.

قال تعالى: ﴿وَمَا أَرْسَلْنَا مِنْ قَبْلِكَ مِنْ رَسُولٍ إِلَّا نُوحِي إِلَيْهِ أَنَّهُ لا إِلَهَ إِلَّا أَنَا فَاعْبُدُونِ﴾ [الانبياء:٢٥].

Allah Anasema: *"Hatukutuma Mtume wa aina yoyote kabla yako isipokuwa Tulimfunulia ya kuwa hapana*

*mola aabudiwaye kwa haki isipokuwa Mimi (Allah) basi niabuduni." (al-An-biyaa: 25).*

*Tauheed* hii ndio ambayo washirikina waliikataa na kuipinga wakati walipolinganiwa na Mitume wa Allah.

قال تعالى: ﴿قَالُوا أَجِئْتَنَا لِنَعْبُدَ اللهَ وَحْدَهُ وَنَذَرَ مَا كَانَ يَعْبُدُ آبَاؤُنَا﴾

[الأعراف:٧٠]

Allah Anasema; *"Wakasema kumuambia Hud, je umetuita tumuabudu Allah Peke Yake, na tuihame ibada ya masanamu ambayo tuliirithi kutoka kwa baba zetu." (al -A'raf:70).*

Haifai kufanya aina yoyote ya ibada kwa asiyekuwa Allah, sio kwa Malaika aliye karibu na Allah, wala Nabii aliyetumwa, wala kwa Walii aliyekuwa mwema, wala yoyoye katika viumbe vyake Allah. Kwani haifai ibada ya aina yoyote kufanywa isipokuwa ifanywe kwa ajili ya Allah.

## 3: *Tauheed Al-Asmaai wa Sswifaat* (Majina Yake Allah na Sifa Zake).

Maana yake ni kuamini Majina yote ambayo Allah Amejiita Yeye Mwenyewe na Kujisifu kwayo, au

aliyoitwa na kusifiwa na Mtume wake Muhammad صلى الله عليه وسلّم. Na kuthibitisha hivyo katika hali ambayo inalingana na Utukufu Wake Allah bila ya kupindisha, wala kukataa ambacho ni wajibu kwake Allah, wala kumfananisha Allah na sifa ya viumbe, katika hali ya uhakika sio majazi. Na kukanusha yale ambayo Allah Yeye Mwenyewe Amekanusha na Kukataa, au zile sifa ambazo Mtume wa Allah amezikanusha na kuzikataa. Na zile ambazo hazijathibitishwa wala kukataliwa ni wajibu mtu kujiepusha nazo, haifai kuthibitisha wala kukanusha.

## Miongoni Mwa Mifano ya Majina Yake Allah.

Allah Anayo Majina Mazuri Aliyojiita Yeye Mwenyewe, kama vile Allah Yuko Hai na Ni wa Tangu. Kwa hiyo ni wajibu kwetu kuamini kuwa Allah Yuko Hai, kwamba Uhai ni miongoni wa Sifa Zake Allah. Nao ni Uhai Uliokamilika ambao haujatanguliwa na kukosekana Uhai, wala kuwa ni Uhai ule unaoisha kwa ukomo.

Allah Amejiita kuwa ni Mwenye Kusikia '*Assami'u*', hapa ni wajibu juu yetu kuamini kuwa Allah - Kusikia ni katika Sifa Yake na ni Jina miongoni mwa Majina Yake *subhanahu wata'ala* na kuwa Allah Anasikia.

قوله تعالى: ﴿وَقَالَتِ الْيَهُودُ يَدُ اللهِ مَغْلُولَةٌ غُلَّتْ أَيْدِيهِمْ وَلُعِنُوا بِمَا قَالُوا بَلْ يَدَاهُ مَبْسُوطَتَانِ يُنْفِقُ كَيْفَ يَشَاءُ﴾ [المائدة:٦٤]

Miongoni mwa Sifa za Allah Anasema: *"Na mayahudi walisema, Mkono wa Allah Umefungwa kutotenda mema, mikono yao ndiyo iliyofungwa, na Allah Amewafukuza kutoka kwenye Rehema Yake kwa sababu ya neno lao hilo, bali Mikono Yake Miwili Imekunjuliwa, Anatoa namna Atakavyo." (al - Maidah: 63)***.**

Allah Anathibitisha kwenye Ayah hii kuwa Anayo Mikono Miwili Iliyosifika kwa Ukunjufu wa Kutoa zaidi Kuwapa waja Wake. Kwa hiyo ni wajibu kuamini hivyo kuwa Allah Anayo Mikono Miwili Yenye Kutoa Iliyojaa Neema mbali mbali, lakini ni lazima kuamini hivyo bila ya kujengea picha kwenye akili zetu, wala ndimi zetu kwa kutamka namna ilivyo hiyo Mikono Miwili ya Allah na kuifananisha na mikono ya viumbe Vyake.

قال تعالى: ﴿لَيْسَ كَمِثْلِهِ شَيْءٌ وَهُوَ السَّمِيعُ الْبَصِيرُ﴾ [الشورى:١١]

*Allah Anasema: "Allah hana mfano wake na chochote, na yeye ni Mwenye Kusikia na Kuona."* *(Al-shurah: 11).*

Ufupi wa maneno katika aina hii ya *Tauheed*, ni kwamba ni wajibu juu yetu kuyathibitisha yote Aliyoyathibitisha Allah Yeye Mwenyewe, au yale aliyoyathibitisha Mtume wake Muhammad, na kuyakataa yale ambayo Allah Mwenyewe Ameyakataa au kukataliwa na Mtume wake Muhammad kutokana na Majina Yake Allah na Sifa Zake, bila ya kubadilisha, wala kufananisha au kupinga sifa miongoni mwa Sifa Zake Allah na kulinganisha.

## Maana ya Kalimat *Tauheed* "*Laailaaha Illallah*"

*Kalimat "Laa ilaaha Illa Llah"* ndio msingi wa Dini. Neno hili lina nafasi kubwa sana katika Dini ya Kiislamu. Kwani ndio nguzo ya kwanza katika nguzo za Uislamu. Pia ni sehemu katika sehemu za Imani, na kukubalika kwa matendo mema kwa kutamkwa *Laa ilaha Illa Llah*, kujua maana yake na kufanyia kazi muktadha wake.

Ama maana ya haki ambayo haifai kupindisha ni "Hapana Mwenye Kuabudiwa kwa Haki Ila Allah", nayo ni Kumpwekesha Allah Peke Yake katika Ibada, na kuacha Ibada isiyokuwa ya Allah.

Miongoni mwa makosa katika kuitafsiri kauli hii kauli ni ni kusema kwamba maana ya *Laa ilaaha Illa Llah*, ni 'hapana muumba isipokuwa ni Allah', au 'hapana muweza au hapana alieanzisha isipokuwa ni Allah', au 'hakuna yeyote mwenye kupatikana isipokuwa ni Allah.'

**Nguzo za *Kalimat Laa ilaaha Illa Lllah*.**

Neno hili lina nguzo mbili;

1. Nguzo ya kwanza ni kukataa.
2. Nguzo ya pili ni kukubali na Kuthibitisha.

Nguzo ya kwanza kukataa, ni kauli ya kusema *"Laa ilaaha"* nako ni kukataa uungu wa kila kitu hapa duniani chenye kuabudiwa kinyume na Allah.

Pili kukubali na kuthibitisha ya kuwa hakuna mola isipokuwa ni Allah Peke Yake Asiyekuwa na mshirika.

Hakuna mola anayepaswa kuabudiwa isipokuwa Allah na wala haifai kufanya chochote katika aina za Ibada kwa asiyekuwa Allah. Kwani mwenye kulisema neno hili la *Laa ilaaha Illa Allah* akalijua maana yake na akaujua muktadhwa wake: Ya kuwa ni kujiepusha na shirki na kuthibitisha Upweke Wake Allah pamoja na kuliitakidi kisawasawa ndani ya moyo wake na kulifanyia kazi. Basi huyo atakuwa ni Muislamu wa kweli.

Lakini mwenye kulifanyia kazi neno hili bila ya kuitakidi kwenye moyo wake, basi huyo atakuwa mnafiki, na mwenye kufanya kinyume ya hayo atakuwa mshirikina na kafiri hata kama atalisema hili neno kwenye ulimi wake.

## Ubora wa *Kalimat Tauheed*

Neno hili "*Laa ilaaha Illa Llah*" lina fadhila kubwa na faida nyingi, miongoni mwa fadhila zake;

1. Neno hili ni sababu ya kumzuia mtu asikae milele motoni, kwa yule anayestahiki kuingia motoni miongoni mwa watu wa *Tauheed*.

ففي الحديث أنَّ رسول الله -ﷺ- قال: ((يخرج من النار من قال: لا إله إلا الله، وفي قلبه وزنُ شعيرةٍ من خيرٍ، ويخرج من النار من قال: لا إله إلا الله، وفي قلبه وزن بُرَّةٍ من خير، ويخرج من النار من قال: لا إله إلا الله، وفي قلبه وزن ذَرة من خير)) [متفق عليه: ٤٤، ١٩٣].

Katika Hadithi ya Bwana Mtume anasema: "*Atatoka motoni yule mwenye kuitamka kalima ya Laa ilaaha Illa Llah, na ndani ya moyo wake ana uzito wa chembe ndogo - mfano wa Shairi - ya kheri, na atatoka motoni yule mwenye kuitamka kalima ya Laa ilaaha Illa Llah, na ndani ya moyo wake ana uzito wa chembe ndogo - mfano wa punje ya ngano Burra - ya kheri na atatoka motoni mwenye kusema Laa ilaaha Illa Llah na kwenye moyo wake kuna punje ndogo – mfano wa sisimizi - kidudu kiduchu- Dharra - ya kheri.*" *(Ameipokea Bukhari na Muslim)*.

2. Kwa ajili ya neno hili la *Tauheed*, Allah Amewaumba majini na wanadamu, Allah Anasema:

قال الله تعالى: ﴿وَمَا خَلَقْتُ الْجِنَّ وَالْإِنسَ إِلَّا لِيَعْبُدُونِ﴾ الذاريات: ٥٦

*"Sikuwaumba majini na wanadamu isipokuwa kwa lengo la kuniabudu."* (*adh-Dhariyat:56*). (Yaani kunipwekesha)

3. Kwa neno hili Allah Aliwatuma Mitume Wake na Akateremsha vitabu kwa Mitume.

قال تعالى: ﴿وَمَا أَرْسَلْنَا مِنْ قَبْلِكَ مِنْ رَسُولٍ إِلَّا نُوحِي إِلَيْهِ أَنَّهُ لا إِلَهَ إِلَّا أَنَا فَاعْبُدُونِ﴾ [الانبياء:٢٥]

Allah Anasema: *"Hatukutuma Mtume yoyote kabla yako, isipokuwa Tulimfunulia kwa kumpatia kitabu ya kwamba hakuna mola apasae kuabudiwa kwa haki isipokuwa Mimi, basi Niabuduni."* (Al-Anbiyah: 25).

4. Neno hili ndio lilikuwa ufunguo wa Mitume kwenye Da'awa yao. Ndilo neno la kwanza katika kulingania mitume, kila Mtume alisema kuwaambia watu.

﴿... يَا قَوْمِ اعْبُدُوا اللهَ مَا لَكُمْ مِنْ إِلَهٍ غَيْرُهُ﴾ [الأعراف:٥٩]

*"Enyi watu muabuduni Allah, hamna nyinyi Mungu mwingine zaidi Yake Yeye."* (Al-A'araf: 59).

## Masharti ya *Kalima* - *Laa ilaaha Illa Llah*.

*Kalima* ya *Laa ilaaha Illa Llah* inayo masharti saba, haifai mpaka yakusanyike masharti yote pamoja, na ashikamane nayo mtu bila ya kuacha hata sharti moja. Miongoni mwa masharti hayo ni;

1. **Elimu** (kujua), maana yake ni kukataa na kuthibitisha kwa yale yanayolazimika mtu kuyafanyia kazi. Mtu atakapoelewa kuwa Allah Ndiye Anayestahiki Kuabudiwa Pekee, na kwamba ibada yoyote ifanywayo kinyume na kumkusudia Allah ni batili haifai. Basi mtu huyo atakuwa ameifahamu maana halisi ya hili neno la *Laa ilaaha Illa Llah*.

قال تعالى:﴿فَاعْلَمْ أَنَّهُ لا إِلَهَ إِلَّا اللهُ﴾ [محمد:١٩].

Allah Anasema: *"Basi tambua na kujua ya kwamba hapana mola apasae kuabudiwa kwa haki isipokuwa ni Allah Peke Yake."* (Muhammad: 19).

Hadithi ilipokelewa na Uthman, Mtume anasema:

وعن عثمان بن عفان ﵁، عن النبي ـ Û ـ قال: ((من مات وهو يعلم أنه لا إله إلا الله دخل الجنة)) [مسلم: ٢٦].

*"Yeyote atakayekufa hali ya kuwa anajua ya kwamba hakuna mola apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah Pekee ataingia peponi."* (Amepokea Imamu Muslim).

2. **Yakini**, ni pale mtu kuitamka shahada kwa yakini iliyotulia moyoni mwake, bila ya kuingiwa na shaka inayowekwa na shetani wa kijini au wa kibinadamu, bali aiseme shahada akiwa na yakini ya kisawasawa.

قال الله تعالى: ﴿إِنَّمَا الْمُؤْمِنُونَ الَّذِينَ آمَنُوا بِاللهِ وَرَسُولِهِ ثُمَّ لَمْ يَرْتَابُوا﴾ [الحجرات: ١٥].

Allah Anasema: *"Hakika si vinginevyo waumini wa kweli ni wale ambao wamemuamini Allah na Mtume Wake, kisha wakawa hawana shaka yoyote."* (al-Hujurat: 15).

وعن أبي هريرة ـ﵁ـ أن رسول الله ـﷺـ قال: ((أشهد أن لا إله إلا الله وأني رسول الله، لا يلقى الله بهما عبدٌ غيرَ شاكٍّ فيهما، إلا دخل الجنة)) [رواه مسلم:٢٧].

Hadithi aliyoipokea Abu Huraira, Radhi za Allah ziwe juu yake, Mtume anasema*: "Mwenye kushuhudilia ya kuwa hapana mola apasae kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah, na akushuhudilia ya kwamba mimi ni Mtume wa Allah, akawa mtu si mwenye shaka juu ya maneno mawili haya, isipokuwa jaza yake ni kuingia peponi."* (Ameipokea Imamu Muslim).

3. **Kukubali:-** Ni kuwa ukubali moyo na ulimi wake mtu kwamba kila ambacho kimeamriwa na neno hili, basi asadikishe kwa kuelezwa, aamini kwa kila kilichokuja kutoka kwa Mtume, na ayakubali hayo yote bila ya kuacha chochote kutoka kwake Mtume, Allah Anasema:

قال الله تعالى: ﴿ آمَنَ الرَّسُولُ بِمَا أُنْزِلَ إِلَيْهِ مِنْ رَبِّهِ وَالْمُؤْمِنُونَ كُلٌّ آمَنَ بِاللهِ وَمَلائِكَتِهِ وَكُتُبِهِ وَرُسُلِهِ لا نُفَرِّقُ بَيْنَ أَحَدٍ مِنْ رُسُلِهِ وَقَالُوا سَمِعْنَا وَأَطَعْنَا غُفْرَانَكَ رَبَّنَا وَإِلَيْكَ الْمَصِيرُ﴾ [البقرة:٢٨٥ ]

*"Ameamini Mtume wa Allah, yale aliyoletewa kwa njia ya wahyi kutoka kwa Mola Wake, na waumini pia wameamini, kila mmoja katika wao amemuamini Allah ya kuwa Ana Malaika, Ameteremsha Vitabu na Ametuma Mitume, na hatukanushi yeyote katika Mitume bali tunawaamini wote, na wanasema tumesikia na tumetii, tunatarajia Msamaha Wako*

*Mola wetu, na Kwako Pekee ndio marejeo."* (al-Baqarah: 285).

Na hayatakubaliwa kwa yule ambae atapinga baadhi ya hukumu za kisheria, kama vile kusimamisha hukumu ya haddi kwa wale ambao walioiba na kuzini. Kupinga mtu kuoa wake zaidi ya mmoja, kupinga mirathi ya kiislamu na mengi mengineyo ya kisharia.

قال تعالى: ﴿وَمَا كَانَ لِمُؤْمِنٍ وَلا مُؤْمِنَةٍ إِذَا قَضَى اللهُ وَرَسُولُهُ أَمْرًا أَنْ يَكُونَ لَهُمُ الْخِيَرَةُ مِنْ أَمْرِهِمْ﴾ [الأحزاب:٣٦]

Allah Anasema: *"Haipaswi kwa muumini mwanaume wala muumini mwanamke, iwapo Allah na Mtume wake Wametoa Uamuzi wataenda kinyume nao."* (Al – Ahzab: 36).

4. **Kufuata:** Kufuata ni kujisalimisha. Na huko kufuata ni kwa lililojulishwa kwenye ***Laa ilaaha Illa Llah***. Tofauti ya Kufuata na kukubalika, ni kwamba kukubalika ni kudhihirika kwa jambo na kukubalika maana yake. Ama kufuata ni kufuatisha jambo kwa kufanya kwa vitendo.

Mwenye mapungufu, ni mtu yeyote atakaejua maana ya *Laa ilaaha Illa Llah* akaiyakinisha moyoni mwake na kuikubali lakini akaacha kuifuata. Pia Mtu mwenye

kuitangaza, kujisalimisha na kufanyia kazi muktadha wa yale aliyoyajua kwenye hili neno la *Laa ilaaha Illa Llah* lakini akawa wakati huo huo hajahakikisha sharti la kufuata, basi pia atakuwa na mapungufu kwenye kuifuata *Laa ilaaha Illa Llah*.

قال الله تعالى: ﴿وَأَنِيبُوا إِلَى رَبِّكُمْ وَأَسْلِمُوا لَهُ﴾ [الزمر:٥٤]

Allah Anasema; *"Na rejeeni kwa Mola wenu na mjisalimishe Kwake."* (Az-zumar: 53).

وقال تعالى: ﴿فَلا وَرَبِّكَ لا يُؤْمِنُونَ حَتَّى يُحَكِّمُوكَ فِيمَا شَجَرَ بَيْنَهُمْ ثُمَّ لا يَجِدُوا فِي أَنْفُسِهِمْ حَرَجًا مِمَّا قَضَيْتَ وَيُسَلِّمُوا تَسْلِيمًا﴾ [النساء:٦٥].

Allah Anasema: *"Naapa kwa Nafsi Yake Allah Mtukufu, ya kwamba hawataamini kikweli mpaka wakufanye wewe ni hakimu wao kwenye ugomvi unaotokea baina yao, kisha wasiingiwe na dhiki katika nafsi zao kwa matokeo ya hukumu yako, na wajisalimishe kisawa sawa."* (An-Nisaa: 65).

5. **Ukweli,** na huo ukweli ni mtu kusadikisha kwenye Imani yake, kusadikisha kwenye *aqeeda* yake, kama ambavyo Anasema Allah:

قال تعالى: ﴿يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا اتَّقُوا اللهَ وَكُونُوا مَعَ الصَّادِقِينَ﴾

[التوبة:١١٩]

*"Enyi Mlioamini mcheni Allah na kuweni pamoja na watu wakweli."* (At-Taubah: 119).

Na Mtume anasema:

وقال ـ Û ـ: ((من شهد أن لا إله إلا الله صادقًا بها دخل الجنة))

[رواه أحمد، وصححه الألباني]

*"Mwenye Kushuhudia ya kwamba hakuna mola anayepaswa kubudiwa kwa haki isipokuwa ni Allah, akawa ni mwenye kusadikisha Laa ilaaha Illa Lllah ataingia peponi."* (Ameipokea Imamu Ahmad na akaisahihisha Al Bani).

Na atakapoitamka shahada kwa ulimi wake, akaikadhibisha kwenye moyo wake, basi haitamsaidia, bali ataingia na kuhesabiwa miongoni mwa watu wanafiki.

Miongoni mwa mambo yanayozuia ukweli ni kuyakadhibisha yale aliyokuja nayo Bwana Mtume au baadhi yake. Kwani Allah Ametuamrisha kumtii Mtume Wake na kumsadikisha, Akafungamanisha na kumtii Yeye pale Aliposema Allah:

قال تعالى: ﴿قُلْ أَطِيعُوا اللهَ وَأَطِيعُوا الرَّسُولَ﴾ [النور:٥٤]

*"Mtiini Allah na mumtii Mtume."* (An-Nur: 54).

6. ***Ikhlas***, ni kutakasa mwanadamu matendo yake mema kwa nia njema, kutokana na chembechembe za kishirikina. Kwa kufanya matendo yake yote ya maneno au ya vitendo yawe ni kwa ajili ya Allah na kutafuta Radhi Zake tu. Asiyafanye kwa kujionesha kwa watu, au asemwe, au anafanya kwa kutaka manufaa fulani, au lengo maalumu, au anafanya kwa matamanio yaliyo wazi au yaliyojificha, au anamkingia mtu kwa ajili ya mapenzi, madhehebu, kundi lisilokuwa kwenye muongozo wa Allah. Bali hapana budi yote atakayoyafanya ayafanye kwa kutafuta Radhi za Allah na Malipo Yake kesho Akhera, hatafuti kulipwa na mtu yeyote wala kushukuriwa na mtu.

قال الله تعالى: ﴿أَلَا للهِ الدِّينُ الخَالِصُ﴾ [الزمر:٣]

Allah Anasema: *"Jua na kutambua ya kuwa Allah Peke Yake Ndie Mwenye Dini iliyotakasika."* (Az-Zumar: 3).

وقال سبحانه: ﴿وَمَا أُمِرُوا إِلَّا لِيَعْبُدُوا اللهَ مُخْلِصِينَ لَهُ الدِّينَ﴾ البينة:٥

Anasema Allah: *"Na hawakuamrishwa katika sharia zote zilizopita isipokuwa ni wamuabudu Allah Peke Yake, hali ya kumtakasia Yeye Dini."* (Al-Bayyinah: 5).

Na imekuja kwenye sahihi mbili, Bwana Mtume anasema:

وفي الصحيحين من حديث عِتبان قوله ـ Û ـ: ((فإنَّ الله قد حَرَّم على النار من قال لا إله إلا الله، يبتغي بذلك وجه الله)) [متفق عليه: ٤٢٥، ٣٣].

*"Hakika ya Allah Ameharamisha moto kumuunguza mwenye kusema Laa ilaha Illa Llah akitafuta Radhi za Allah."* (Ameipokea Bukhar na Muslim).

7. **Mapenzi:** Ni kuipenda *Laa ilaha Illa Llah* na kila ambacho kinafungamana na hili neon. Na ampende Allah na Mtume wake, na atangulize mapenzi ya kumpenda Allah na Mtume wake kuliko kitu chochote kile. Ampende Allah mapenzi yanayo fungamana na Utukufu Wake, na Ukubwa Wake, na Khofu Yake, na atarajie mema kutoka Kwake Allah. Na azipende sehemu zote Anazozipenda Allah kama vile Makka, Madina na misikiti yote iliyopo duniani. Na azipende nyakati na zama kama vile mwezi wa Ramadhan, Masiku kumi ya mwezi wa *Dhul Hijja* na masiku mengine. Na awapende viumbe watukufu kama vile

Manabii, Mitume, Malaika wote, waja wema na Mashahidi. Na pia apende matendo mema kama vile Swala, Zakat, Swaumu na Hijjah. Na pia apende dhikri za kumtaja Allah na apende kusoma Qur'an.

Na miongoni mwa mapenzi kwa Allah ni kutakunguliza kila aina ya mapenzi Kwake Allah kuliko mapenzi ya nafsi yake mtu pamoja na matamaniwa yake. Pia achukie kila ambacho Allah Anakichukia, achukie ukafiri, ufasiki na uovu wa aina yoyote. Allah Anasema:

قال الله تعالى:﴿ يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا مَنْ يَرْتَدَّ مِنْكُمْ عَنْ دِينِهِ فَسَوْفَ يَأْتِي اللهُ بِقَوْمٍ يُحِبُّهُمْ وَيُحِبُّونَهُ أَذِلَّةٍ عَلَى الْمُؤْمِنِينَ أَعِزَّةٍ عَلَى الْكَافِرِينَ يُجَاهِدُونَ فِي سَبِيلِ اللهِ وَلا يَخَافُونَ لَوْمَةَ لائِمٍ﴾ [المائدة:٥٤].

*"Enyi mlioamini, yeyote kati yenu atakayerudi nyuma akaiacha Dini yake, basi Allah Atawaleta watu bora kuliko wao, Anaowapenda na wanaompenda, wenye huruma kwa waumini, wakali kwa makafiri, wanapigana jihadi na maadui wa Allah, na hawaogopi lawama za mwenye kulaumu."* (al-Maidah: 54).

## Maana ya Kushuhudia Kuwa Muhammad ni Mjumbe Wake Allah.

Maana yake ni kutambua kwa dhahiri na kwa siri ya kwamba Muhammad ni mja Wake Allah na ni Mtume Wake, Amemtuma kwa ajili ya watu wote. Na kwa kulifanyia kazi hili, ni kumtii Mtume kwa yale yote anayoamrisha, na kumsadikisha kwa yale anayoyaeleza na kujiepusha na yale yote anayoyakataza na kuyakemea. Na kusiabudiwe chochote ila kile ambacho kipo kwenye sharia ya Allah. Na kushuhudia ya kuwa Muhammad ni Mtume Wake Allah, kuna nguzo mbili muhimu ambazo ni;

- **Nguzo ya kwanza** ni Muhammad ni mja wa Allah na Mtume Wake. Nguzo hii inakataza kuchupa mipaka katika haki yake Mtume kuwa yeye ni mja wa Allah na Mtume Wake. Na kuamini ya kuwa yeye Muhammad ni kiumbe aliyekamilika na hizi sifa mbili alizokuwa nazo. Kwani maana ya kuwa ni mja wa Allah, kuwa yeye ni mja mwenye kumilikiwa, kwa hiyo ni mwanadamu aliyeumbwa miongoni mwa viumbe vyake Allah, yanampata kama vile yanayo wapata wengine katika viumbe.

قال تعالى:﴿قُلْ إِنَّمَا أَنَا بَشَرٌ مِثْلُكُمْ ...﴾[الكهف:١١٠ ]

Allah Anasema*: "Sema uwaambie kuwa, hakika si vinginevyo mimi ni mwanadamu mfano wenu."* (Al-Kahf: 110).

Allah Anasema:

وقال سبحانه: ﴿الحَمْدُ لله الَّذِي أَنْزَلَ عَلَى عَبْدِهِ الْكِتَابَ وَلَمْ يَجْعَلْ لَهُ عِوَجَا﴾ [ الكهف:١].

*"Kila sifa njema ni Zake Allah Ambaye Amemteremshia mja Wake kitabu na asikifanye ni chenye kupotoka."* (Al-Kahf: 1).

- **Nguzo ya pili** ni kujua maana ya *Rasuul* (Mjumbe wa Allah), maana yake ni aliyetumwa kwa watu wote kwa ajili ya kulingania kwa ajili ya Allah, kuwabashiria watu mambo ya kheri na kuwaonya watu na mambo ya shari. Na katika kushuhudilia hili katika hizi sifa mbili ambazo ni kukataa kuchupa mipaka katika haki ya Bwana Mtume, kwani wako wengi katika wafuasi wake wanaochupa mipaka katika haki ya Mtume na wakampandisha katika daraja ya juu zaidi. Kwa kumtoa katika nafasi yake ya utume na kumpandisha katika nafasi ya kuabudiwa kinyume ya Allah. Wakamtaka msaada kinyume na Allah, wakamtaka awafanyie mambo asiyokuwa na uwezo nayo isipokuwa Allah Pekee. Katika kuwakidhia haja zao na

kuwaondolea matatizo yao. Na wako wengine ambao walipinga ujumbe aliokuja nao Mtume.

Wako ambao walimfuata Mtume na kumtweza katika haki yake ya wajibu, wakayatanguliza maneno ya waja zaidi kuliko maneno ya Mtume, wakapuuza sunnah za Mtume na wakategemea maneno yanayo kwenda kinyume na aliyokuja nayo Mtume.

# Imaani na Nguzo Zake.

## الإيمان وأركانه

## *Imaan*:

*Imaan* ni maneno, vitendo na Itikadi.

*Imaan* inazidi kwa kuyafanya matendo mema ya kumtii Allah, na Imaan inapungua kwa kufanya matendo mabaya ya kumuasi Allah. *Imaan* ni maneno yaliyomo moyoni na kutamkwa kwa ulimi, na matendo ya moyoni, kwa kutamka kwa ulimi na kafanyiwa kazi na viungo. Kauli ya moyoni ni kuitakidi na kusadikisha moyoni, na kauli ya ulimi ni kukiri. Na matendo ya moyo ni kujisalimisha, kujitakasa na kutangaza, kupenda, kufanya yaliyo mema. Kufanya kazi viungo ni kuyafanya yaliyoamrishwa na kujiepusha na yaliyokatazwa.

Kwa hakika, imewekwa wazi kwenye Qur'an na *Sunnah* za Bwana Mtume ya kwamba *Imaan* ina nguzo zake, ambazo ni;

1: Kumuamini Allah.
2: Kuwamini Malaika wa Allah.
3: Kuamini Vitabu vya Allah.
4: Kuwaamini Mitume wa Allah.
5: Kuamini Siku ya Mwisho.

6: Kuamini *Qadar* ya Allah, kheri na shari vyote ni vya Allah.

قال تعالى:﴿آمَنَ الرَّسُولُ بِمَا أُنْزِلَ إِلَيْهِ مِنْ رَبِّهِ وَالْمُؤْمِنُونَ كُلٌّ آمَنَ بِاللَّهِ وَمَلائِكَتِهِ وَكُتُبِهِ وَرُسُلِهِ لا نُفَرِّقُ بَيْنَ أَحَدٍ مِنْ رُسُلِهِ وَقَالُوا سَمِعْنَا وَأَطَعْنَا غُفْرَانَكَ رَبَّنَا وَإِلَيْكَ الْمَصِيرُ﴾ [البقرة:٢٨٥ ].

Allah Anasema: *"Ameamini Mtume wa Allah, yale aliyoletewa kwa njia ya wahyi kutoka kwa Mola wake, na waumini pia wameamini, kila mmoja katika wao amemuamini Allah ya kuwa Ana Malaika, Ameteremsha vitabu na Ametuma Mitume, na hatukanushi yeyote katika Mitume bali tunawaamini wote, na wanasema tumesikia na tumetii, tunatarajia msamaha wako Mola wetu, na Kwako Pekee ndio marejeo."* (Al-Baqarah: 285).

Na kama ilivyokuja katika sahihi Muslim kutokana na Hadithi ya Amir Muuminina Umar bin Khatwab ya kwamba bwana Mtume anasema:

كما جاء في صحيح مسلم من حديث عمر بن الخطاب ﷺ: (أَنَّ جبريل ـ عليه السلام ـ سأل النبي -ﷺ- عن الإيمان، فقال له: ((الإِيمانُ

أن تؤمنَ بالله، وملائكته، وكتبه، ورسله، واليوم الآخر، وتؤمن بالقدر خيره وشره)) [رواه مسلم:٨].

*"Hakika ya Jibril alimuuliza Mtume kuhusiana na Imaani, Mtume akamjibu akasema, 'Imaan ni kumuamini Allah, na Malaika wake, Kuamini vitabu vyake, kuamini Mitume wake, kuamini siku ya mwisho, na kuamini Qadar yake kheri na shari ni vyake."* (Ameipokea Imamu Muslim).

Kwa haya mambo sita, ndio misingi mikuu ya *Aqeeda* sahihi ambayo iliteremka kwenye Kitabu cha Allah (Qur'an), na ndiyo ambayo alitumilizwa kwayo Bwana Mtume na ndio inayoitwa **Nguzo za Imaan**.

## 1: Nguzo ya Kwanza ya *Imaan* ni Kumuamini Allah.

Kumuamini Allah ni Kumpwekesha Allah katika Uungu Wake, Ulezi Wake, Majina Yake na Sifa Zake.

Miongoni mwa Kumuamini Allah ni;

1: Kuamini kuwa Allah Ndiye Mwenye Kustahiki ibada Peke Yake, kwa kuwa Yeye Ndiye Muumba wa viumbe wote, Aliyewafanyia ihsani, Anayewa simamia Riziki Zake na Anayejua siri zao na dhahiri

zao, Mwenye Uwezo wa Kuwalipa thawabu wenye kumtii na kuwaadhibu wenye kumuasi.

Na uhakika wa hilo ni kuwa Imaani ni Kumpwekesha Allah katika yote Anayostahiki kuabudiwa katika aina zote za ibada. Katika hali ya unyenyekevu, katika kupenda na kuwa na hofu juu ya Allah, pamoja na mapenzi ya dhati kwa Allah na kujidhalilisha katika Utukufu Wake Allah.

Kuhusu msingi mkubwa ulioshuka Qur'an, Allah Anasema:

قال تعالى:﴿فَاعْبُدِ اللهَ مُخْلِصًا لَهُ الدِّينَ أَلا للهِ الدِّينُ الخَالِصُ﴾ [الزمر:٢-٣]

*"Muabudu Mola wako kwa kumtakasia Yeye Dini, zindukeni hakika Allah Ndiye Mwenye Dini iliyotakasika."* (Az-Zumar: 2-3).

وقوله: ﴿ وَقَضَى رَبُّكَ أَلَّا تَعْبُدُوا إِلَّا إِيَّاهُ ﴾ [الاسراء:٢٣]

Allah Anasema: *"Amehukumu Mola wako ya kuwa msiabudu chochote isipokuwa Yeye tu Peke Yake..."* (Al-Israh: 23).

Zipo aina nyingi za ibada, miongoni mwa ibada hizo ni; Kuomba dua, kuwa na khofu, kuwa na matarajio

mazuri kwa Allah, kumtegemea Allah, kuwa na raghaba na uoga, kunyenyekea, kuogopa, kurejea kwa Allah, kutaka msaada, kujikinga, kuchinja, kuweka nadhiri. Na nyinginezo katika aina za ibada ambazo haifai kuzifanya ibada hizi kinyume na Allah. Na atakaefanya ibada miongoni mwa ibada hizi kwa asiyekuwa Allah atakuwa amemshirikisha Allah na kukufuru.

Ushahidi wa dalili ya kuwa Dua ni ibada, Allah Anasema:

قوله تعالى:﴿ وَقَالَ رَبُّكُمُ ادْعُونِي أَسْتَجِبْ لَكُمْ إِنَّ الَّذِينَ يَسْتَكْبِرُونَ عَنْ عِبَادَتِي سَيَدْخُلُونَ جَهَنَّمَ دَاخِرِينَ﴾ [غافر:٦٠]

*"Amesema Mola wenu; Niombeni Nitazijibu dua zenu, hakika wale ambao wanafanya kiburi cha kutoniomba, wataingia moto wa jahanamu hali ya kuwa ni wadhalilifu."* (Ghafir: 60).

وفي الحديث ما رواه النعمان بن بشير ﵁، عن النبي - Û - أنَّه قال:

((الدُّعَاءُهوَ العِبَادَةَ)) [رواه الترمذي: ٢٩٦٩].

Na hadithi aliyoipokea Nu'uman bin Bashir kutoka kwa Mtume Rehema na amani zimfikie anasema: "*Dua ndio Ibada*." (Ameipokea Tirmidhiy).
Dalili ya hofu ni Kauli Yake Allah Aliposema:

قال تعالى: ﴿فَلاَ تَخَافُوهُمْ وَخَافُونِ إِن كُنتُم مُّؤْمِنِينَ﴾ آل عمران:١٧٥

*"Msiwaogope hao niogopeni Mimi, ikiwa nyinyi ni waumini wa kweli."* (Al- Imran: 175).

Dalili ya kutarajia kukutana na Allah ni Neno Lake Allah Aliposema:

قال تعالى: ﴿فَمَن كَانَ يَرْجُو لِقَاء رَبِّهِ فَلْيَعْمَلْ عَمَلاً صَالِحاً وَلَا يُشْرِكْ بِعِبَادَةِ رَبِّهِ أَحَدًا﴾ [الكهف:١١٠].

*"Basi yeyote anayetarajia kukutana na Allah, basi afanye matendo mema na asimshirikishe Allah kwenye ibada yake na yeyote."* (Al-Kahf: 110).

Dalili ya ku-*Tawakkal*, Allah Anasema:

قال تعالى:﴿وَعَلَى اللهِ فَتَوَكَّلُواْ إِن كُنتُم مُّؤْمِنِينَ﴾ [المائدة:٢٣]

*"Na kwa Allah mtegemeeni ikiwa nyinyi ni waumini."* (al-Maidah: 23).

وقوله: ﴿وَمَن يَتَوَكَّلْ عَلَى اللهِ فَهُوَ حَسْبُهُ﴾ [الطلاق:٣].

Allah Anasema tena: *"Na yeyote atakae mtegemea Allah basi Yeye Atamtosheleza."* (at-Talaq: 3).

Dalili ya *Raghaba* (matumaini ya kupata mazuri) na *Rahabah* (khofu), *Khushu'u* (unyenyekevu), Allah Anasema:

قال تعالى:﴿ إِنَّهُمْ كَانُوا يُسَارِعُونَ فِي الخَيْرَاتِ وَيَدْعُونَنَا رَغَبًا وَرَهَبًا وَكَانُوا لنَا خَاشِعِينَ﴾ [الأنبياء:٩٠].

*"Kwa kweli wao walikuwa wakiikimbilia kila kheri wakitumai kupata mazuri yaliyopo Kwetu wakiogopa mateso Yetu na walikuwa wadhalilifu na wanyonge Kwetu."* (al-Anbiyaa: 90).

Dalili ya *Khashiya* (kuogopa) Allah Anasema:

قوله تعالى﴿ :فَلاَ تَخْشَوْهُمْ وَاخْشَوْنِي﴾ [البقرة:١٥٠].

*"Basi msiwaogope niogopeni Mimi."* (Al-Baqara: 150).

Na dalili ya Kurejea kwa Allah ni:

قوله تعالى: ﴿وَأَنِيبُوا إِلَى رَبِّكُمْ وَأَسْلِمُوا لَهُ﴾ [الزمر:٥٤].

*"Na rejeeni kwa Mola wenu enyi watu, kwa kutii na kutubia na mnyenyekeeni..."* (Az-Zumar: 54).

Na dalili ya kuomba Msaada kwa Allah:

قوله تعالى: ﴿ إِيَّاكَ نَعْبُدُ وَإِيَّاكَ نَسْتَعِينُ ﴾ [الفاتحة:٥]

*"Kwako Wewe tu tunakuabudu na Kwako Wewe tu tunakuomba msaada."* (al-Fatihah: 5).

وقوله ﷺ:((إِذَا اسْتَعَنْتَ فَاسْتَعِنْ بِاللهِ)) [رواه الترمذي: ٢٥١٦]

Na Mtume Rehema na Amani Zimfikie anasema: *"Unapotaka kuomba msaada basi taka msaada kwa Allah."* (Ameipokea Tirmidhiy 2516).

Dalili ya Kujikinga kwa Allah:

قَوْلُهُ تَعَالَى: ﴿ قُلْ أَعُوذُ بِرَبِّ النَّاسِ﴾ [الناس:١].

*"Sema ewe Muhammad najikinga kwa Mola wa watu."* (An-Nas: 1).

Dalili ya Kuomba kupata msaada (*Istighaathat*) Allah Anasema:

قوله تعالى: ﴿إِذْ تَسْتَغِيثُونَ رَبَّكُمْ فَاسْتَجَابَ لَكُمْ﴾ [الأنفال:٩].

*"Mkumbukeni Mola wenu wakati mlipomuomba Allah mpate ushindi kwa maadui wenu, Allah Akakubali maombi yenu..."* (al-Anfal: 9).

Dalili ya Kuchinja, Allah Anasema:

قوله تعالى﴿ :قُلْ إِنَّ صَلاتِي وَنُسُكِي وَمَحْيَايَ وَمَمَاتِي لله رَبِّ الْعَالَمِينَ لاَ شَرِيكَ لَهُ وَبِذَلِكَ أُمِرْتُ وَأَنَاْ أَوَّلُ الْمُسْلِمِينَ﴾ [الأنعام:١٦٣].

*"Sema ewe Mtume, hakika Swala yangu, na kuchinja kwangu na uhai wangu na kufa kwangu ni kwa ajili ya Allah Mola wa viumbe wote. Asiye na mshirika katika Uungu Wake, huko ndiko niliko amrishwa na mimi ni wa kwanza kumfuata Allah."* (Al-An'am:162).

Na miongoni mwa dalili za *Sunnah* za Mtume katika kuchinja ni;

قوله ﷺ:((لَعَنَ اللهُ مَنْ ذَبَحَ لِغَيْرِ اللهِ)) [رواه مسلم: ١٩٧٨].

*"Allah Amemlani mwenye kuchinja kinyume cha Allah."* (Ameipokea Imam Muslim).

Na dalili katika kuweka *Nadhiri*, Allah Anasema:

قوله تعالى: ﴿يُوفُونَ بِالنَّذْرِ وَيَخَافُونَ يَوْمًا كَانَ شَرُّهُ مُسْتَطِيرًا﴾

[الإنسان:٧].

*"Wanatekeleza Nadhiri walizoziweka, na wakiogopa siku ya kiyama ambayo madhara yake ni hatari na ubaya wake ni wenye kusambaa na kuenea kwa watu."* (Al-Insan: 7).

Iwapo mazoea pindi yatakapokusudiwa uchamungu na kumtii Allah kama vile kulala, kula, kunywa, kutafuta riziki, kuoa na mengineyo, na mtu akayafanya mazoea hayo kwa nia njema basi itakuwa ni ibada kwake na atalipwa Muislam ujira na thawabu juu yake.

2: Miongoni mwa kumuamini Allah ni kuamini yote Aliyoyawajibisha na Kuyalazimisha kufanywa katika ibada Zake. Na Akafaradhisha juu ya waja Wake katika nguzo tano za Uislamu za dhahiri ambazo ni:- kutoa shahada, ya kwamba hapana mola wa kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah na kushuhudia ya kuwa Muhammad ni mjumbe Wake na Mtume Wake, kusimamisha Swala tano, kutoa Zaka, kufunga mwezi wa Ramadhan na kwenda kuizuru nyumba tukufu ya Makkah (Al-Ka'aba) kwa mwenye uwezo wa kwenda huko. Pamoja na kutekeleza faradhi nyingine zilizokuja kwenye shariah tukufu ya Allah.

3: Na katika kumuamini Allah ni kuamini ya kuwa Allah Ndiye Aliyeumba ulimwengu na Kuyaendesha mambo ya walimwengu wote kwa Ujuzi Wake na Uwezo Wake Atakavyo Yeye. Na kwamba Yeye Ndiye Mmiliki wa dunia na akhera, Mlezi wa viumbe wote, hakuna muumbaji zaidi Yake, hakuna Mola Mlezi zaidi Yake, Yeye Ndiye Aliwatuma Mitume wote, Ameteremsha Vitabu kwa lengo la kuwafanyia mazuri

waja Wake kwa kuwalingania kwenye mambo ambayo kwao yana masilahi ya kufaulu duniani na akhera.

Kwa hayo yote Allah Hana mshirika, kama Alivyosema;

قال تعالى: ﴿اللَّهُ خَالِقُ كُلِّ شَيْءٍ وَهُوَ عَلَى كُلِّ شَيْءٍ وَكِيلٌ﴾[الزمر:٦٢]

*"Allah Mdiye Muumba wa vitu vyote, na ni Mtunzi wa kila kitu."* (Az-Zumar: 62).

4: Katika *Imaan* ya Kumuamini Allah, ni kuyaamini Majina Yake Mazuri na Sifa Zake Zilizotukuka. Zilizoelezwa katika Kitabu Chake Kitukufu ambacho ni Qur'an na kuthibitishwa na Mtume Wake Muaminifu Muhammad Rehema na Amani zimfikie. Bila ya kupindisha wala kuacha sifa yoyote, wala kubadilisha wala kufananisha na sifa ya kiumbe yeyote.

Pamoja na kuamini yale yenye maana tukufu kuwa ni miongoni mwa Sifa Zake Allah ambazo ni wajibu kusifiwa kwa kuendana Naye zisizofanana na sifa za kiumbe yeyote Aliyemuumba, kama Anavyosema Allah;

قال تعالى: ﴿لَيْسَ كَمِثْلِهِ شَيْءٌ وَهُوَ السَّمِيعُ الْبَصِيرُ﴾ [الشورى:١١].

*"Hana mfano na chochote Allah, na Yeye Anasikia na kuona."* (Ashurah: 11).

## 2: Nguzo ya Pili ni Kuamini Malaika wa Allah.

Inakusanya nguzo hii kuwaamini Malaika wote kwa pamoja na kuamini Malaika hawa kwa ufafanuzi zaidi.

Ama kuamini Malaika wote kwa pamoja, ni kuamini ya kwamba Allah Anao Malaika Aliowaumba kwa ajili ya kumtii Yeye tu, na hao Malaika wako aina nyingi, miongoni mwao ni;

- Malaika wanaobeba *'Arsh* ya Allah
- Malaika wa peponi na motoni
- Malaika waliowakilishwa kwa kuhifadhi matendo ya waja.

Ama katika njia ya ufafanuzi, tunaamini ya kuwa wale aliowaita majina yao Allah na Mtume Wake kama vile Malaika Jibril, Malaika Mikail, na Malaika Mwenye kumiliki khazina za Motoni na Israfil aliye wakilishwa katika kupuliza parapanda.

Malaika hawa Allah Amewaumba kwa nuru kama ilivyothibiti kutoka katika Hadithi ya mama Aisha, Allah Amridhie, mkewe Mtume Muhammad, Rehema na Amani Zimfikie, aliyoipokea Imamu Muslim, Mtume anasema:

عن عائشة ـ Û ـ أنَّ النبي ـ ﷺ ـ قال: (( خُلقت الملائكة من نور، وخُلق الجان من مارج من نار، وخُلق آدم مما وُصِفَ لكم)) [رواه مسلم:٢٩٩٦].

*"Wameumbwa Malaika kwa Nuru na wameumbwa Majini kutokana na ndimi za moto na ameumbwa Adam kutoka na yale mliyoelezewa."*

## 3: Nguzo ya Tatu ni Kuamini Vitabu vya Allah.

Ni wajibu kuamini moja kwa moja ya kuwa Allah Ameteremsha Vitabu kwa Manabii Wake na Mitume Wake ili Kubainisha haki kwa waja Wake na Kulingania kwa kutumia hivyo Vitabu.

Tuamini katika njia ya ufafanuzi kwa Aliyoyasema Allah, miongoni mwa vitabu hivyo ni Taurat, Injili, Zabur na Qur'an. Na Quran ndio kitabu cha mwisho kuteremshwa, kimekuja kutilia nguvu na kuvisadikisha vitabu vilivyotangulia.

Kwa hiyo ni wajibu kwa watu wote kuifuata Qur'an na kuitolea hukumu katika mambo yao yote na kutumia yale yote yaliyo kuwa sahihi katika mafundisho ya Mtume Muhammad, Rehema na Amani Zimfikie, kwani Allah Amemtumiliza Mtume Muhammad, Rehema na Amani Zimfikie, kwa viumbe wa aina mbili (*Athaqalaini* - Majini na Binadamu) na akateremshiwa hii Qur'an ili awahukumu baina yao.

Allah Akaifanya Qur'an kuwa ni pozo (dawa) kwa yale yote yaliyomo vifuani mwa waja na ni ufafanuzi wa kila kitu, na ni muongozo na ni rahma kwa watu wote. Allah Anasema:

قال تعالى: ﴿وَهَذَا كِتَابٌ أَنْزَلْنَاهُ مُبَارَكٌ فَاتَّبِعُوهُ وَاتَّقُوا لَعَلَّكُمْ تُرْحَمُونَ﴾ [الأنعام:١٥٥]

*"Na hiki kitabu Tumekiteremsha kimebariki -wa, basi kifuateni na mcheni Allah ili mpate kurehemewa."* (Al – Ani'am:155).

Allah Anasema:

وقال سبحانه: ﴿وَنَزَّلْنَا عَلَيْكَ الْكِتَابَ تِبْيَاناً لِكُلِّ شَيْءٍ وَهُدىً وَرَحْمَةً وَبُشْرَى لِلْمُسْلِمِينَ﴾ [النحل:٨٩]

*"Tumekuteremshia Kitabu kiwe ni upambanuzi wa kila jambo na ni muongozo na ni rahma na bishara njema kwa waislamu."* (An-nahl: 89).

## 4: Nguzo ya Nne ya Imaani ni Kuamini Mitume wa Allah.

Ni wajibu kuwaamini Mitume wote kwa pamoja na kwa upambanuzi, tuamini ya kwamba Allah Amewatuma Mitume kwa waja Wake. Kwani Mitume ni wenye kubashiria watu mambo mema na kuwaonya watu na mambo maovu wao ni walinganiaji kwenye haki. Allah Anasema;

قال تعالى: ﴿وَلَقَدْ بَعَثْنَا فِي كُلِّ أُمَّةٍ رَسُولاً أَنِ اعْبُدُوا اللهَ وَاجْتَنِبُوا الطَّاغُوتَ ... ﴾ [النحل:٣٦]

*"Kwa hakika Tulituma kwa kila umma Mtume, kuwaambia watu wake wamuabudu Allah na wajiepushe na twaghuti (Shetani)."* (An-Nahl: 36).

Mwenye kuitikia wito wa Mitume atafaulu na kusalimika, na mwenye kupinga wito wao ataangamia na kujuta.

Tunaamini kuwa ulinganiaji wa Mitume wote ni mmoja, ni ulinganiaji wa kumpwekesha Allah katika

ibada, lakini walikhitilafiana kwenye hukumu na sharia zao walizopewa na Allah.

Tunaamini kuwa wako Mitume bora kati yao, na mbora wao kati ya hao wote ni Mtume wa mwisho Muhammad Rehema na Amani Zimfikie. Allah Anasema:

قال الله سبحانه: ﴿وَلَقَدْ فَضَّلْنَا بَعْضَ النَّبِيِّينَ عَلَى بَعْضٍ﴾ [الاسراء:٥٥]

*"Na kwa hakika Tumewafadhilisha baadhi ya Mitume juu ya wengine."* (Al Israh: 55).

وقال سبحانه: ﴿ مَا كَانَ مُحَمَّدٌ أَبَا أَحَدٍ مِنْ رِجَالِكُمْ وَلَكِنْ رَسُولَ اللهِ وَخَاتَمَ النَّبِيِّينَ﴾ [الأحزاب:٤٠].

Allah Anasema: "*Hakuwa Muhammad ni baba wa mmoja katika waume zenu, lakini ni Mtume wa Allah na ni mwisho wa Mitume*." (Al-Ahzab: 40).

Na wale ambao Allah Amewataja miongoni mwao au Akathibitisha Mtume Wake majina yao, tunawaamini kwa ufafanuzi na kuelezwa kama vile Mtume Nuhu, Hud, Swaleh, Ibrahim na wengineo pamoja na mbora wa Mitume Muhammad Rehema na Amani Zimfikie.

## 5: Nguzo ya Tano Kuamini Siku ya Mwisho.

Nguzo hii inaingia ndani yake kila ambacho Allah Amekieleza Yeye na Mtume Wake Rehema na Amani Zimfikie, katika yale ambayo yatakuwa baada ya kufa, fitna za kaburi, adhabu za kaburi na neema za kaburi. Na yale yatayotokea siku ya kiyama kutokana na vituko vyake na shida za siku hiyo.

Na kupita kwenye *Swiratwa* (njia Maalum), Mizani, Hisabu na malipo, na kugaiwa watu vitabu vya matendo yao baina ya watu. Yupo atakayechukua kitabu chake kwa mkono wa kulia, na mwengine atachukua kitabu chake kwa mkono wa kushoto kwa kutokea nyuma ya mgongo.

Kwenye nguzo hii pia kunaingia *Imaan* ya kuamini kuwa kuna birika (Hodhi) aliloandaliwa kunywa maji yake, Mtume wetu Muhammad, Rehema na Amani Zimfikie. Kwani kila Mtume analo birika lake, kama ilivyokuja katika hadithi za Mtume, Rehema na Amani Zimfikie. Pia katika nguzo hii inaingia *Imaan* ya kuamini pepo na moto, waumini kumuona Mola wao siku ya Kiyama na Kuwasemesha na mengineyo kama ilivyokuja kwenye Qur'an na *Sunnah* za Mtume, Rehema na Amani Zimfikie. Ni wajibu kuyaamini hayo yote na kuyasadiki katika hali ambayo Ameibainisha Allah na Mtume Wake.

## 6: Nguzo ya Sita ni *Qadar*.

Na katika nguzo hii kunakusanyika mambo makuu manne;

a) **Jambo la Kwanza**: Allah Anayajua yaliyotangulia na yatakayokuwa baadae. Anazijua hali za waja Wake kuanzia riziki zao, ajali zao, matendo yao na mengineyo katika mambo yao hakuna kilichojificha Kwake Allah. Allah Anasema:

قال سبحانه: ﴿إِنَّ اللهَ بِكُلِّ شَيْءٍ عَلِيمٌ﴾ [التوبة:١١٥].

*"Hakika ya Allah juu ya kila kitu ni Mjuzi."* (At-Tawbah: 115).

b) **Jambo la Pili**: Kuamini kuwa kila Alichokiandika Allah Amekikadiria na Kukidhibiti hukumu yake. Allah Anasema:

قال سبحانه: ﴿وَكُلَّ شَيْءٍ أَحْصَيْنَاهُ فِي إِمَامٍ مُبِينٍ﴾ [يس:١٢].

*"Hakika kila kitu Tumekidhibiti katka kitabu chenye ufafanuzi."* (Yasin: 12).

c) **Jambo la Tatu**: Kuamini Matakwa Yake Allah (*Mashiatun*) yaliyotekelezwa tokea zamani. Alitakalo Allah linakuwa na Asilolitaka haliwi. Allah Anasema:

قال سبحانه: ﴿كَذَلِكَ اللهُ يَفْعَلُ مَا يَشَاءُ﴾ [آل عمران:٤٠].

*"Hivyo basi Allah Anafanya Atakavyo."* (al Imran: 40).

**Jambo la Nne**: Kuamini ya kuwa Allah Ndiye Aliyeumba yaliyokadiriwa kabla ya kutokea. Allah Anasema:

قال سبحانه: ﴿وَاللهُ خَلَقَكُمْ وَمَا تَعْمَلُونَ﴾ [الصافات:٩٦]

*"Na Allah Ndiye Aliyewaumbeni nyinyi na yale mnayoyatenda."* (As-swafat: 96).

# Shirki na Aina Zake

## الشرك وأنواعه

**Shirki** ni mja kumfanyia Allah kwa kumshirikisha na mungu mwingine kinyume Naye katika Ulezi Wake, Uungu Wake na Majina Yake na Sifa Zake.

**Shirki Ziko Aina Mbili**;

- Shirki kubwa
- Shirki ndogo

**Shirki Kubwa.**

Shirki kubwa ni kufanya aina yoyote ya ibada kwa mwingine kinyume na Allah. Na mwenye kufanya shirki atakaa motoni milele ikiwa atakufa bila ya kutubia kwa Allah. Shirki inabatilisha matendo mema ya mtu. Allah Anasema:

قال تعالى: ﴿وَلَوْ أَشْرَكُوا لَحَبِطَ عَنْهُمْ مَا كَانُوا يَعْمَلُونَ﴾ [الأنعام:٨٨]

*"Na lau kama watamshirikisha Allah, basi yatapomoka yote waliyokuwa wakiyafanya."* (Al - Anam: 88).

Na shirki kubwa Allah Haisamehe isipokuwa mtu mpaka atubie toba ya kisawaswa.

قال تعالى: ﴿إِنَّ اللهَ لا يَغْفِرُ أَنْ يُشْرَكَ بِهِ وَيَغْفِرُ مَا دُونَ ذَلِكَ لِمَنْ يَشَاءُ وَمَنْ يُشْرِكْ بِاللهِ فَقَدِ افْتَرَى إِثْماً عَظِيمًا﴾ [النساء:٤٨].

Allah Anasema: "*Hakika ya Allah Hataisamehe dhambi ya kushirikishwa, na Anayasamehe madhambi mengine yasiyokuwa shirki, na mwenye kumshirikisha Allah kwa hakika amezua dhambi kubwa sana.*" (An-Nisaa: 48).

Miongoni mwa aina za Shirki kubwa ni kuomba kwa asiyekuwa Allah, au kuweka nadhiri kwa asiyekuwa Allah. Au kuchinja kwa asiyekuwa Allah, au kufanya kwa asiyekuwa Allah miungu mingine na kuipenda zaidi ya Allah na vinginevyo.

قال تعالى:﴿وَمِنَ النَّاسِ مَنْ يَتَّخِذُ مِنْ دُونِ اللهِ أَنْدَادًا يُحِبُّونَهُمْ كَحُبِّ اللهِ﴾ [البقرة:١٦٥] .

"*Wako miongoni mwa watu wanachukua badala ya Allah miungu mingine, wakiwapa mapenzi kama wanavyo mpenda Allah.*" (Al-Baqarah: 165).

## Shirki Ndogo.

Shirki ndogo ni ile ambayo imeelezwa kwenye Qur'an au Hadithi za Mtume Muhammad, Rehema na Amani

za Allah Zimfikie, akasema kuwa ni shirki lakini ikawa haijafika kiwango cha Shirki kubwa.

Shirki hii ndogo haimtoi mtu katika Uislamu tofauti na Shirki kubwa lakini inapunguza katika kumpwekesha Allah. Mfano wa Shirki hii ndogo ni, kama vile mtu kuwa na Riya, na kauli ya kusema Ametaka Allah na wewe na kusema lau si kama Allah na wewe. Pia kuapa kwa asiyekuwa Allah, bila ya kuitakidi kuwa kinachoapiwa kinanufaisha au kinadhuru kinyume ya Allah.

Pia kusema kuwa Akitaka Allah na kutaka fulani basi jambo hili lingekuwa hivi hivi n.k.

لقول النبي ﷺ: ((أَخوفُ ما أَخافُ عليكم الشرك الأصغر))، فسُئل عنه،

فقال: ((الرياء)) [رواه أحمد وإسناده جيد]

Mtume Rehema na Amani Zimfikie anasema: *"Kitu cha kuwahofisha zaidi juu yenu ni Shirki ndogo." Akaulizwa Mtume, 'ni ipi hiyo?' Mtume akasema, "ni Mtu kuwa na Riya."* (Ameipokea Imamu Ahmad na Mapokezi yake ni mazuri).

وقوله ﷺ: ((منْ حَلفَ بغير الله فقد أشرك)) [رواه أبو داود: ٢٨٢٩].

Mtume Rehema na Amani Zimfikie anasema: *"Mwenye kuapa kinyume ya Allah, kwa hakika*

*amefanya shirki."* (Ameipokea Imam Abu Daud: 2829).

Matendo yanayofungamana na Shirki ndogo ni kufunga hirizi, kufunga bangili au uzi kwa lengo la kukuondolea madhara au kukukinga na maradhi pamoja na matatizo. Na mtu atapoitakidi kuwa inamnufaisha au kumdhuru na kwamba ndio sababu ya kudhurika au kunufaika, basi hapo ataingia kwenye Shirki kubwa.

# Itikadi ya Kundi Lililo Faulu.

## مجمل اعتقاد الفرقة الناجية

Itikadi ya kundi lililofaulu ndio itikadi ya *Ahlu sunnah wal Jamaa.* Nayo ni itikadi ya kuamini haki, kushuhudia kuwa Allah Peke Yake Ndiye Anayestahiki Kuabudiwa, Aliye Pweke kwa Ukamilifu, Mwenye Kuabudiwa na Kutakasiwa Yeye Pekee Dini. Na kuelewa ya kuwa Allah Pekee Ndiye Muumbaji, Muanzilishi wa Uumbaji, Anayewapa sura viumbe Wake kulingana na Hekima Yake, Mwenye kutoa riziki, Mwenye Sifa ya Kutoa, Mwenye Sifa ya Kuzuia, Mwenye Sifa ya Kuendesha mambo yote ya viumbe Wake.

Na hakika Yeye Allah Ndiye Anayestahiki Kuabudiwa kwa haki. Na Yeye Ndiye wa Mwanzo hakuna baada Yake chochote, Yeye Ndiye wa Mwisho hakuna baada yake chochote, Yeye Yupo hakuna juu Yake chochote, na Yeye Amejificha hakuna chini Yake chochote.

Na kwamba Allah Yupo juu ya kila kitu, hakuna juu Yake chochote zaidi Yake. Kwa maana Yake halisi na mazingatio, Allah Yupo juu kwa Dhati Yake, Uwezo Wake na Nguvu Zake.

Na kwa hakika Allah Yupo juu ya A'arshi Yake Ametulia, Kutulia kunakolingana na Utukufu na Ukubwa Wake Allah. Ujuzi Wake Allah Umeenea kila kitu dhahiri na batini. Allah ni Mjuzi wa Kujua yaliyo juu na chini. Anawajua waja Wake vizuri, Anazijua hali zao zote. Na Yeye Yupo karibu kujibu dua zao wanapomuomba.

Hakika ya Allah ni Mkwasi, Ametosheka Si Muhitaji kwa viumbe Vyake vyote. Na viumbe vyote Kwake ni masikini, ni viumbwa na vyote wanavyovihitajia nyakati zote pia vimeumbwa.

Hakuna chochote katika viumbe Vyake chenye kujitosheleza hata kiasi cha kupepesa jicho. Na Yeye Allah ni Mpole Mwenye Huruma. Hakuna kwa waja Wake neema ya aina yoyote ya Dini wala ya dunia isipokuwa inatoka Kwake Yeye. Yeye Ndiye Mwenye Kuleta hizo neema na Ndiye Anayeondoa na Kuwakinga na mabalaa.

Kutokana na Huruma Zake Allah, Anateremka Kuja mbingu ya dunia wakati ikibaki thuluthi ya mwisho ya usiku.

فيقول: ((منْ ذا الذي يسألني فأعُطيَه، من ذا الذي يستغفرني فأغفرَ له))

حتى يطلع الفجر، فهو ينزل نزولًا يليق به جل شأنه.

"*Ni nani mwenye kuniomba Nimpe, ni nani mwenye kunitaka msamaha Nimsamehe, hali inakuwa hivyo mpaka kuchomoza kwa Alfajir na Kuteremka Kwake Allah Kunalingana na Utukufu Wake."*

Allah ni Mwingi wa Hikma iliyopea katika Sharia Zake na Qadari Yake. Hakuumba chochote bure wala hakuweka sheria isipokuwa kwa maslahi ya waja Wake na Kuwaepusha na mabaya.

Allah ni Mwingi wa Kukubali toba na Kusamehe. Allah Anakubali toba za waja Wake na Anasemehe makossa yao. Anasamehe makosa makubwa kwa Mwenye kutubia na kurejea Kwake.

Allah ni Mwenye Kushukuru, Anashukuru kidogo katika matendo ya mja, na Anamlipa malipo makubwa na mengi na Anawazidishia zaidi kwa wale wenye kumshukuru kutokana na Fadhila Zake.

Muumini wa kweli anaelezea Sifa za Allah vile Alivyojisifu Mwenyewe na Alivyosifiwa na Mtume Wake katika Sifa za Dhati Yake na Sifa za Vitendo. Kama vile Sifa ya Uhai Uliyokamili, Sifa ya Kusikia na Kuona, Sifa ya Ukamilifu wa Uwezo, Utukufu na Kibri, Sifa ya Utukufu, Uzuri na Ukamilifu pamoja na Sifa zote nzuri zinazomstahiki Yeye Allah.

Muumini anaamini yote yaliyokuja kwenye kitabu cha Allah na kufuatiliwa na *Sunnah* za Bwana Mtume Muhammad, Rehema na Amani Zimfikie. Kwa kuwa waumini watamuona Mola wao siku ya kiyama peponi kwa macho ya wazi kabisa, ni Neema kumuona Allah, na kufaulu kwa kupata Radhi Zake ni neema kubwa zaidi na ladha kubwa ya peponi.

Na yeyote mwenye kufa bila ya kuwa na *Imaan* na *Tauheed*, basi mtu huyo atakaa milele katika moto wa Jahannam. Na wenye madhambi makubwa miongoni mwa waumini pindi wanapokufa bila ya kutubia, wataingia motoni lakini hawatadumu humo na wala hatabakia motoni yeyote ambaye kwenye moyo wake kuna chembe ndogo ya *Imaan* isipokuwa atatolewa humo.

*Imaan* inakusanya itikadi ya moyo kauli na matendo, matendo ya viungo na maneno ya ulimi. Mtu atakayesimamia katika njia iliyokamilika basi huyo atakuwa muumini wa kweli ambaye anastahiki malipo mema na kusalimika na adhabu ya moto. Kwani imaani inazidi na kupungua. Inazidi imaani kwa kufanya mambo mema na inapungua imaani kwa kutenda maasi na mambo mabaya.

Kama anavyoshuhudia muumini kuwa Muhammad Rehema na Amani Zimfikie ni mja wa Allah na Mtume Wake, Allah Amemtumiliza kwa muongozo na Dini ya

haki ili iweze kushinda dini nyingine zote. Na yeye Mtume ni kiumbe bora kuliko waumini wote na nafsi zao. Na yeye ni mwisho wa Mitume. Ametumwa kwa majini na watu wote kuja kuwabashiria mema na kuwaonya kufanya mambo ya shirki na maovu. Ametumwa pia alinganie kwa Allah kwa Idhini Yake, awe ni taa yenye kuangaza. Ametumwa kuirekebisha Dini na dunia ili viumbe wote wasimame kwenye haki ya kumuabudu Allah Peke Yake, Asiye na mshirika. Na wamtake msaada Allah katika kutafuta rizki. Na watambue kuwa Allah Anawajua zaidi viumbe Wake. Allah ni Mkweli zaidi, Ana nasaha nzuri zaidi na ni Mtukufu Aliye wazi katika Kauli. Amtukuze Allah na ampende, atangulize mapenzi yake juu ya kupenda viumbe wote. Wamfuate Allah katika misingi ya Dini na matawi yake, waitangulize Kauli Yake na Muongozo Wake juu ya kauli na muongozo wa wengine wote.

Na aitakidi mja kuwa Allah Amemkusanyia fadhila na mambo maalumu kwa ukamilifu jambo ambalo Hajalifanya kwa kiumbe yeyote zaidi ya Mtume Muhammad Rehema na Amani Zimfikie. Na Mtume ni kiumbe mwenye nafasi ya juu zaidi kwa Allah, na ana cheo kikubwa zaidi, na ni mkamilifu wa fadhila. Kwani hakuna kheri yoyote isipokuwa aliujulisha umma wake na hakuna shari isipokuwa aliutahadharisha umma wake kutokana na shari hiyo.

Muumini anatakiwa aamini kila kitabu Alichokiteremsha Allah na kila Mtume Aliyemtuma Allah anayejulikana na asiyejulikana. Muumini wa kweli habagui kati ya Mitume wa kuwaamini, kwa kuwa ujumbe wao ni mmoja, nao ni kumuabudu Allah Mmoja Asiye na mshirika.

Vile vile muumini anatakiwa aamini *Qadar.* Kwani matendo yote wayafanyayo waja ya kheri au ya shari yote Allah Anayajua na Allah Kishapitisha Kalamu Yake, na yameshatekelezwa Matakwa Yake kufungamana na Hikma Yake. Allah Amewaumba viumbe Wake kwa Uwezo Wake na Matakwa Yake, sio kwa matakwa yao ya kauli zao na vitendo vyao. Hawakumlazimisha Allah kuwa Awafanyie watakavyo, bali Allah Aliwaumba kwa kutaka Kwake.

Allah Amewachagua waumini na Akawapenda kwa kuwapambia *Imaan* kwenye nyoyo zao, na kuwafanya wauchukie ukafiri, uovu na maasi kwa Uadilifu Wake na Hikma Yake.

Miongoni mwa misingi ya *Aqeeda* ni pale muumini anapojipamba na Dini, kwa kunasihiwa kwa ajili ya Allah, na Kitabu Chake na Mtume Wake na viongozi wa ummah na waislamu wote. Muumini aamrishe mema na akataze mabaya juu ya yale ambayo ni wajibu katika shariah ya Uislamu. Kwa kuwafanyia

wema wazazi wawili, kuunga undugu na kuwafanyia ihsani jamaa wa karibu katika familia pamoja na majirani wenye haki na wewe. Na kuwafanyia ihsani viumbe wote. Alinganie kwenye tabia njema na mazuri ya tabia njema, na akataze kulingania katika mambo maovu na mabaya.

Na awe anaitakidi kuwa ukamilifu wa imaani na yakini ya muumini, ni kwa yule ambaye anafanya matendo mema na kuwa na tabia njema na kuwa mkweli. Na kuwaongoza watu katika njia ya kheri na kuwakataza kuiendea njia ya shari.

Muumini wa kweli ni yule ambaye anatambua kuwa jihadi katika njia ya Allah ipo inaendelea mpaka siku ya kiyama. Na Jihadi ndio muhimili mkuu wa Dini ya Kiislamu. Kuna Jihadi ya elimu na hoja. Jihadi ya kupigana kwa silaha, na hii ni faradhi kwa kila Muislamu kuilinda Dini yake kwa njia yoyote anayoweza kupigana. Na kila kiongozi wa ummah anatakiwa kuitangaza awe ni kiongozi mwema au muovu aitangaze Jihadi pale yatakapotimia masharti yake na sababu zake.

Na miongoni mwa misingi ya Dini ya Kiislamu ni kutilia umuhimu umoja wa Kiislamu. Kwa kuzikurubisha nyoyo za Waislamu kuwa pamoja na kuwatahadharisha na ubaya wa kutengana na

kuchukiana bila ya sababu. Na kuwakataza kuwaudhi viumbe wengine kwa kumwaga damu zao, kuchukua mali zao bila ya haki, na kuwavunjia heshima zao na haki zao. Pia kuamrisha uadilifu katika muamiliano wao pamoja kati ya waislamu na wasiokuwa waislamu.

Kama vile ambavyo anaitakidi Muumini kuwa ummah bora ni ummah wa Mtume wetu Muhammad, Rehema na Amani Zimfikie. Na Maswahaba bora ni Maswahaba wa Mtume Muhammad Rehema na Amani Zimfikie. Hasa hasa Makhalifa wanne, pamoja na wale kumi waliobashiriwa pepo na Mtume Muhammad Rehema na Amani Zimfikie na wale *Ahlul Badri* (waliopigana vita vya Badri) na wale waliomkubali Mtume na kumsapoti katika *Bai'atul Ridh -wan* na wale Maswahaba wa mwanzo waliongia kwenye Uislamu miongoni mwa Muhajirina na Answar. Ni wajibu kuwapenda maswahaba wa Mtume Rehema na Amani Zimfikie. Kuwapenda ni sehemu ya Dini. Kueneza kwa kuutangaza wema wao Maswahaba na kunyamaza kuyatangaza na kuyasema mabaya yao pia ni sehemu ya Dini na Kuwapenda.

Ni katika Dini kuwaheshimu wanavyuoni na viongozi waadilifu katika watawala. Na wale ambao wana nafasi za juu katika Dini, na wale wenye heshima mbali mbali katika Waislamu. Tumuombe Allah Awalinde na shari,

shaka, ushirikina, kuwagawa Waislamu, unafiki na tabia mbaya. Awathibitishe katika Dini ya Mtume wao mpaka siku ya mwisho ya mauti.

Hii ndio misingi mikuu inayofuatwa na kundi lililofaulu na misingi hii ndio inayofuatwa na wafuasi wake na kwayo wanailingania kwa watu waifuate misingi hii.

# Fihrisi ya Kitabu

Misingi ya Aqeedah. ..........................................3
*Tauheed* na Aina Zake..........................................3
1: *Tauheed Ar-Rububiyyah*. ..................................4
2: *Tauheed Al-Uluhiyyah*. ....................................7
3: *Tauheed Al-Asmaai wa Sswifaat* (Majina Yake Allah na Sifa Zake). ..............................................8
Maana ya Kalimat *Tauheed*................................12
Nguzo za *Kalimat Laa ilaaha Illa Lllah*. .................12
Ubora wa *Kalimat Tauheed*................................14
Masharti ya *Kalima* - *Laa ilaaha Illa Llah*. .............16
Maana ya Kushuhudia Kuwa Muhammad ni Mjumbe Wake Allah. ...................................................25
Imaani na Nguzo Zake. .......................................28
1: Nguzo ya Kwanza ya *Imaan* ni Kumuamini Allah. ...................................................................30
2: Nguzo ya Pili ni Kuamini Malaika wa Allah. .......39
3: Nguzo ya Tatu ni Kuamini Vitabu vya Allah. .....40
4: Nguzo ya Nne ya Imaani ni Kuamini Mitume wa Allah. ..........................................................42
5: Nguzo ya Tano Kuamini Siku ya Mwisho. .........44
6: Nguzo ya Sita ni *Qadar*..................................45
Shirki na Aina Zake .........................................47
Itikadi ya Kundi Lililo Faulu. ................................51